BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2019

# KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2019

# KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA ........................................ 1

2.1 Sehemu A: Sarufi ........................................................................... 2

2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi ......................................................... 28

2.3 Sehemu C: Ushairi ........................................................................ 42

2.4 Sehemu D: Utungaji ...................................................................... 51

2.5 Sehemu E: Ufahamu ...................................................................... 55

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI ................................................................ 64

4.0 HITIMISHO ........................................................................................ 65

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ................................................................ 66

KIAMBATISHO A ...................................................................................... 67

KIAMBATISHO B ...................................................................................... 69

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili mwaka 2019. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu.

Taarifa hii inaonesha mafanikio ya mfumo wa elimu kwa ujumla hasa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu ni uthibitisho dhahiri wa namna mfumo wa elimu ulivyofanikiwa au ulivyoshindwa kuwapa watahiniwa maarifa yaliyotarajiwa katika kipindi cha miaka saba.

Taarifa hii inaweka bayana sababu zilizochangia baadhi ya watahiniwa kufaulu na wengine kushindwa. Sababu za watahiniwa kufaulu ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali za somo la Kiswahili, jambo linalothibitisha kuwa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ulifanyika vizuri. Kwa upande mwingine sababu za watahiniwa kushindwa ni kama vile; kutoelewa maana za msamiati, kutoelewa matakwa ya swali na kukosa maarifa kuhusu kanuni za lugha katika kuunda sentensi zenye muundo sahihi kisarufi. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia maelezo, jedwali na vielelezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu stahiki zitakazoboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wahitimu watapata ujuzi na maarifa yanayotakiwa na kuwawezesha

kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mazingira yao baada ya Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na Wataalam wa TEHAMA kwa kushiriki ipasavyo katika uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani ulikuwa na maswali **arobaini na tano** (**45)** ambapo maswali **arobaini (40)** ni ya kuchagua jibu sahihi na kila swali lilikuwa na alama **moja (01)**. Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu **nne (04)** kama ifuatavyo: Sehemu A *Sarufi*; B *Lugha ya Kifasihi*; C *Ushairi* na D *Utungaji*. Aidha, kulikuwa na maswali **matano (05)** ya kujieleza kutoka sehemu E *Ufahamu* ambayo yalikuwa na alama **mbili (02)** kwa kila swali.

Jumla ya watahiniwa **947,077** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2019** somo la Kiswahili na waliofanya mtihani walikuwa **933,323**. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni **813,283** sawa na asilimia **87.13**.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umefanyika kwa kuainisha maswali yote ya mtihani, ambayo ni yale ya kuchagua herufi ya jibu sahihi na yale ya majibu mafupi. Uchambuzi huu unaonesha majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali kwa kuzingatia idadi na asilimia ya watahiniwa waliochagua kila chaguo. Uchambuzi wa takwimu umewasilishwa kwa njia ya jedwali na vielelezo. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha viwango vya kufaulu na asilimia ya watahiniwa kwa kila swali ambapo, rangi nyekundu imetumika kuwawakilisha kiwango hafifu cha kufaulu yaani **0 – 39,** rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani cha kufaulu yaani asilimia **40 – 59** na rangi ya kijani imetumika kuwakilisha kiwango kizuri cha kufaulu yaani asilimia **60 – 100**. Aidha, alama ***** imetumika katika jedwali na vielelezo kuonesha jibu sahihi lililotakiwa kwa kila swali. Vilevile, watahiniwa ambao wamechagua jibu zaidi ya moja au hawakufanya chaguo lolote wameoneshwa kwa neno “mengine”.

## 2.1 Sehemu A: Sarufi

Sehemu hii ilikuwa na maswali ishirini (20) yaliyomtaka mtahiniwa kuonesha uwezo wa kutambua aina za maneno, maana ya misamiati, matumizi ya nafsi, wakati, hali na kauli mbalimbali za vitenzi.

**Swali la 1:** "Ziara ya Rais Obama ilikuwa ya heri." Neno "ziara" ni aina gani ya neno?

A Nomino

B Kielezi

C Kitenzi

D Kihisishi

E Kivumishi.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 1 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 1: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 412,047 | 230,986 | 166,845 | 28,120 | 91,737 | 3,588 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 44.15 | 24.75 | 17.88 | 3.01 | 9.83 | 0.38 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 412,047 sawa na asilimia 44.15 walichagua jibu sahihi A *Nomino.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya dhana ya Nomino ambayo hutaja majina ya watu, vitu au mahali hivyo, kuweza kubaini neno *ziara* kuwa ni nomino au jina.

Aidha, watahiniwa 521,276 sawa na asilimia 55.85 hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina mbalimbali za maneno hivyo, walichagua vipotoshi ambavyo ni B *Kielezi*, C *Kitenzi* D *Kihisishi* na E *Kivumishi.* Watahiniwa waliochagua *kielezi,* walishindwa kutambua kuwa neno hilo halitoi taarifa juu ya nomino bali huelezea zaidi kuhusu kitenzi. Pia, uteuzi wa *kitenzi* unatokana na watahiniwa kuhusisha dhana ya neno "ziara" na utendekaji wa jambo hivyo kufananisha na *kitenzi,* neno linalotaja tendo. Vilevile, uteuzi wa *kihisishi* unaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa kuwa kihisishi ni neno ambalo linaonesha vionjo vya moyo na kugusa hisia za watu. Aidha, uteuzi wa *kivumishi* unaonesha kuwa watahiniwa hawakufahamu kwamba *kivumishi* ni neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno.

**Swali la 2:** "Msanii huyu anaimba ovyo." Neno "ovyo" ni aina gani ya neno?

A Kivumishi

B Kitenzi

C Kihisishi

D Nomino

E Kielezi.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na.2 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 2: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 240,919 | 91,874 | 50,852 | 54,882 | 491,422 | 3,374 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 25.81 | 9.84 | 5.45 | 5.88 | 52.65 | 0.4 |

Kiwango cha kufaulu kilikuwa cha wastani, ambapo watahiniwa 491,422 sawa na asilimia 52.65 walichagua jibu sahihi E, *Kielezi* kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na hivyo kuweza kubaini kuwa neno "*ovyo"* ni kielezi ambacho kinaelezea zaidi kuhusu kitenzi kilivyofanyika.

Watahiniwa 441,901 sawa na sailimia 47.35 walichagua vipotoshi ambavyo ni A *Kivumishi,* B *Kitenzi,* C *Kihisishi, na* D *Nomino.* Watahiniwa waliochagua *Kivumishi,* walishindwa kuelewa kuwa kivumishii hueleza zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi na si jinsi tendo lilivyofanyika. Aidha, uteuzi wa *kitenzi* unatokana na watahiniwa kuhusisha dhana ya neno "ovyo" na utendekaji wa jambo hivyo, kufananisha na *kitenzi,* neno linalotaja tendo. Vilevile, uteuzi wa *kihisishi* unaonesha kuwa watahiniwa walihusisha neno "ovyo" na "kihisishi," neno ambalo huonesha vionjo vya moyo na kugusa hisia za watu badala ya kuonesha namna tendo lilivyofanyika. Pia, uteuzi wa *nomino*, neno linalotaja majina ya watu, vitu au mahali ulitokana na kuhusisha na jambo lililotendwa na mtenda badala ya kuonesha namna jambo lilivyotendwa yaani *kielezi.* Uteuzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa, watahiniwa hao hawakufahamu maana ya kivumishi, kitenzi, kihisishi na nomino hivyo kushindwa kubainisha aina ya neno katika sentensi.

**Swali la 3:** "Upole wake umemponza." Katika sentensi hii "upole" ni aina gani ya neno?

A Kiwakilishi

B Kivumishi

C Nomino

D Kielezi

E Kitenzi

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 3 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 3: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 163,996 | 279,326 | 282,786 | 153,191 | 49,743 | 4,281 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 17.57 | 29.93 | 30.30 | 16.41 | 5.33 | 0.46 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 650,537 sawa na asilimia 69.70 walichagua vipotoshi: A *Kiwakilishi*, B *Kivumishi*, D *Kielezi* na E *Kitenzi*. Uteuzi wa *kiwakilishi* ulitokana na watahiniwa kuhusisha na dhana ya neno linalosimama badala ya nomino kwa kuwa lilikuwa mwanzoni mwa sentensi hiyo. Aidha, uteuzi wa *kivumishi* ulitokana na kuhusisha neno "upole" na sifa ya kitu/mtu kama kivumishi, kutokana na kutoelewa kuwa, neno hilo huelezea zaidi nomino au kiwakilishi katika sentensi. Waliochagua *kielezi,* walishindwa kubaini kuwa, neno hilo hutumika kuelezea zaidi kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Vilevile, waliochagua *kitenzi* walishindwa kubaini kuwa ni neno linaloarifu juu ya ufanyikaji wa tendo. Kwa jumla uteuzi wa

vipotoshi hivyo umetokana na watahiniwa kukosa uelewa kuhusu aina za maneno hususani, nomino dhahania.

Hata hivyo, watahiniwa 282,786 sawa na asilimia 30.30 walichagua jibu sahihi C, *Nomino* kwa kuwa walikuwa na marifa ya kutosha kuhusu aina za maneno na aina za nomino na hivyo kubaini kuwa neno “upole” ni nomino dhahania.

**Swali la 4:** Asalalee! Tumekwisha. Neno “Asalalee!” ni la aina ipi?”

A Kitenzi

B Kihisishi

C Nomino

D Kivumishi

E Kihusishi.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno kama yalivyotumika katika sentensi. Jedwali Na. 4 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na.4: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 45,413 | 705,692 | 61,400 | 64,063 | 52,928 | 3,827 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 4.87 | 75.61 | 6.58 | 6.86 | 5.67 | 0.41 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 705,692 sawa na asilimia 75.61 walichagua jibu sahihi B *Kihisishi*. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kihisishi ambacho ni neno linaloonesha vionjo vya moyo na kugusa hisia za watu.

Watahiniwa 227,631 sawa na asilimia 24.39 walichagua vipotoshi A *Kitenzi*, C *Nomino*, D *Kivumishi* na E *Kihusishi*. Uteuzi wa *kitenzi*

ulitokana na kushindwa kubaini kuwa neno hilo huarifu juu ya ufanyikaji wa tendo, uteuzi wa *nomino* ulitokana na kuhusisha neno hilo na “nomino” ambayo kimsingi hujitokeza mwanzoni mwa sentensi kutokana na kutokuelewa kuwa *nomino* hutaja majina ya watu, vitu au mahali. Pia uteuzi wa *kivumishi*, neno linaloelezea nomino au kiwakilishi katika sentensi na uteuzi wa *kihusishi*, neno linalohusisha maneno mawili au zaidi yenye hadhi tofauti ulitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa mahususi kuhusu aina za maneno.

**Swali la 5:** Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupiga pasi nguo za watu kwa malipo anaitwaje?

A Dalali


B Dobi

C Kuli

D Bawabu

E Mpambe.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kufahamu maana ya misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 1 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.




*Kielelezo Na. 1: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Asilimia 88.71 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B *Dobi.* Watahiniwa hao wanafahamu kuwa "dobi" ni mtu anayefanya kazi ya kufua nguo za watu kwa malipo.

Uchambuzi wa takwimu za kufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 105,406 sawa na asilimia 11.29 walichagua vipotoshi, A *Dalali,* C *Kuli,* D *Bawabu* na E *Mpambe.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa *Dalali* ni mtu anayenadi na anayeuza vitu mnadani, *Kuli* kuwa ni mtu anayefanya kazi ya kupakia na kupakua shehena za meli au jahazi, *Bawabu* ni mlinzi na *Mpambe* ni mtu anayetumwa kupeleka ujumbe wa sherehe/msimamizi wa maharusi. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu misamiati hiyo inavyotumika katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 6:** Mtu anayecheza mchezo wa kupigana ngumi anaitwaje?

A Mchezaji

B Mkorofi

C Bondia

D Mgomvi

E Mwanamazoezi.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kufahamu maana ya misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 5 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 5: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 25,013 | 44,797 | 769,992 | 39,447 | 50,977 | 3,097 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 2.68 | 4.80 | 82.50 | 4.23 | 5.46 | 0.33 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 769,992 sawa na asilimia 82.50 walichagua jibu sahihi ambalo ni C *Bondia.* Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuweza kubaini kuwa *bondia* ni mtu anayecheza mchezo wa kupigana ngumi.

Watahiniwa 163,331 sawa na asilimia 17.50 walichagua vipotoshi A *Mchezaji,* B *Mkorofi,* D *Mgomvi* na E *Mwanamazoezi.* Uteuzi wa kipotoshi *Mchezaji* yaani mshiriki wa mchezo fulani, *Mkorofi*, mtu mwenye kisirani/matata/mwovu au mwenye udhia, *Mgomvi*, mtu mwenye tabia ya kugombana na watu na *Mwanamazoezi* ni mtu anayefanya mazoezi mara kwa mara, umetokana na watahiniwa hao

kutokuwa na uelewa wa kutosha wa maana ya msamiati katika lugha ya Kiswahili, hususan neno “bondia”.

**Swali la 7:** Kisawe cha neno anuwai ni kipi?

A Chache

B Nyingi

C Kikomo

D Kubwa

E Mbalimbali.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kufahamu maana ya misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 6 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 6: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 158,814 | 152,245 | 227,524 | 54,650 | 332,171 | 7919 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.02 | 16.31 | 24.38 | 5.86 | 35.59 | 0.85 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu, ambapo watahiniwa 601,152 sawa na asilimia 64.41 walishindwa kubaini kisawe cha neno *anuwai* katika chaguzi walizopewa. Watahiniwa hao walichagua kipotoshi A *Chache*, B *Nyingi*, C *Kikomo* na D *Kubwa*. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakufahamu kuwa msamiati “anuwai” una maana sawa na neno *mbalimbali* lenye dhima ya kuonesha utofauti wa vitu.

Aidha, watahiniwa 332,171 sawa na asilimia 35.6 walichagua jibu sahihi E *Mbalimbali* kwa kuwa walikuwa na uelewa wa neno hilo

lenye maana sawa na neno *anuwai* ambayo huwa na dhima ya kuonesha vitu visivyokuwa sawa au tofauti.

**Swali la 8:** Ni neno lipi kati ya maneno yafuatayo lina maana sawa na neno "hamaki"?

A Ghadhabu

B Ghilibu

C Gharibu

D Gharimu

E Ghaibu.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya misamiati katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 7 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 7: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 424,186 | 62,920 | 110,544 | 228,573 | 99,185 | 7,915 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 45.45 | 6.74 | 11.84 | 24.49 | 10.63 | 0.85 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 509,137 sawa na asilimia 54.55 walishindwa kubaini neno lenye maana sawa na neno "hamaki" linalomaanisha *hasira za papo kwa papo/chuki au ghadhabu.* Watahiniwa hao walichagua vipotoshi: B *Ghilibu*, C *Gharibu,* D *Gharimu* na E *Ghaibu.* Watahiniwa waliochagua *Ghilibu*, walishindwa kubaini kuwa neno hilo lina maana ya *shinda kwa hila au danganya, Gharibu* neno lenye maana ya *mtu anayetoka mbali ya eneo fulani/mgeni*. Aidha, uteuzi wa *Gharimu*, linalomaanisha *kutaka kiasi fulani cha malipo/kutiwa matatizoni au kuteketea kwa*


*mali* na *Ghaibu* lenye maana ya *kusoma bila kuangalia maandishi* kulitokana na watahiniwa kukosa uelewa wa maana ya maneno hayo yenye maana tofauti na neno “hamaki.”

Aidha, watahiniwa 424,186 sawa na asilimia 45.45 walichagua jibu sahihi A *Ghadhabu* kwa kuwa waliweza kubaini neno hilo lenye maana sawa na neno “hamaki” kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana za misamiati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 9:** Kinyume cha neno “ukwasi” ni kipi?

A Utajiri
B Ukata
C Uzandiki
D Uzalendo
E Unafiki.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu maana ya misamiati katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 2 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




*Kielelezo Na. 2: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 550,819 sawa na asilimia 59.02 walichagua jibu sahihi B *Ukata* lenye maana ya hali ya kuwa maskini au ufukara ambacho ni kinyume cha neno "ukwasi." Watahiniwa hao walielewa maana ya neno "ukwasi" kuwa ni uwezo mkubwa wa kuwa na mali hivyo, ilikuwa rahisi kwao kuchagua jibu sahihi.

Watahiniwa 382,504 sawa na asilimia 40.98 walichagua vipotoshi A *Utajiri,* C *Uzandiki,* D *Uzalendo na* E *Unafiki*. Uteuzi wa kipotoshi *utajiri* ulitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa neno hilo lina maana sawa na "ukwasi" ambayo yote humaanisha *uwezo* mkubwa wa kuwa na mali, uteuzi wa kipotoshi *uzandiki* ambayo ni hali ya unafiki, uteuzi wa kipotoshi *uzalendo*, hali ya mtu kuipenda

sana nchi yake/kuitetea/uraia au utaifa*, na* uteuzi wa kipotoshi *unafiki* ni hali ya kujifanya kuwa ni rafiki ilihali ni adui. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati husika na hivyo, kushindwa kubaini kinyume cha neno "ukwasi" yaani *ukata*.

**Swali la 10:** "Mavazi yale yalimfanya aonekane __________sana."
Ni neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A nakshi

B nasaha

C nadhiri

D nadhifu

E nathari

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Muhtasari wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo umeoneshwa katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 47,772 | 47,142 | 56,277 | 756,889 | 21,468 | 3,775 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.12 | 5.05 | 6.03 | 81.10 | 2.30 | 0.40 |

Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa, watahiniwa 756,889 sawa na asilimia 81.10 walichagua jibu sahihi D, *nadhifu* linalomaanisha kupendeza. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msamiati *nadhifu* yaani hali ya kuwa safi/ kupendeza/maridadi kama linavyotumiwa katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 176,434 sawa na asilimia 18.90 walichagua vipotoshi: A *nakshi*, B *nasaha*, C *nadhiri* na E *nathari.*

Watahiniwa hao walishindwa kukamilisha sentensi kwa kuchagua kipotoshi *nakshi* kutokana na kutokuelewa kuwa neno hilo lina maana ya urembo wa kuchora, kutarizi au kuchonga; wengine walichagua kipotoshi *nasaha* neno lenye maana ya kumpa mtu mawaidha, mashauri au mwongozo mzuri katika jambo; *nadhiri* inayomaanisha ahadi anayotoa mtu kutimiza kwa Mungu wakati atakapofanikiwa katika jambo. Aidha, uteuzi wa wa kipotoshi *nathari* yenye maana ya maandishi ya moja kwa moja, insha, hadithi au tamthiliya, kulitokana na watahiniwa hao kutojua maana za misamiati hiyo, hivyo kushindwa kubaini neno sahihi linalokamilisha sentensi hiyo yaani "nadhifu" lenye maana ya kuwa safi au kupendeza.

**Swali la 11:** Meli ilitia nanga salama kwani ______________ wetu alikuwa mzoefu. Neno linalokamilisha sentensi hii ni lipi?

A baharia
B dereva
C nahodha
D rubani
E fundi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sarufi* na lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 9 linaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.

**Jedwali Na. 9: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 41,472 | 70,776 | 769,875 | 32,714 | 15,466 | 3,020 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 4.44 | 7.58 | 82.49 | 3.51 | 1.66 | 0.32 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 769,875 sawa na asilimia 82.49 waliweza kuchagua jibu sahihi C *nahodha.* Watahiniwa hao walikuwa na maarifa yakutosha kuhusu maana ya neno “nahodha” kuwa: ni mtu anayeendesha na kuongoza chombo kinachosafiri majini.

Hata hivyo, watahiniwa 163,448 sawa na asilimia 17.51 walichagua vipotoshi A *baharia,* B *dereva,* D *rubani* na E *fundi*. Kipotoshi *baharia* hakikuwa sahihi kwa kuwa, neno baharia humaanisha mfanyakazi wa chombo cha majini, (mwanamaji). Kipotoshi *dereva* hakikuwa sahihi kwa kuwa, neno hilo humaanisha mtu anayefanyakazi ya kuendesha vyombo vya usafiri barabarani. Uteuzi wa kipotoshi *rubani* haukuwa sahihi kwani humaanisha ni mtu anayeendesha ndege na uteuzi wa kipotoshi *fundi* ina maana ya mtu anayefanya kazi kutokana na ujuzi fulani. Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa kuhusu maana za misamiati, hivyo kushindwa kukamilisha sentensi hiyo.

**Swali la 12:** "Nilipokwenda kwake __________ kama tulivyokubaliana." Neno linalokamilisha sentensi hii ni lipi?

A sikumkuta

B nilimkuta hayupo

C ninamkuta

D nitamkuta

E sitamkuta yupo.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Muhtasari wa majibu ya watahiniwa umeoneshwa katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Idadi na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo**

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 683,887 | 102,553 | 46,479 | 75,637 | 20,682 | 4,085 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 73.27 | 10.99 | 4.98 | 8.10 | 2.22 | 0.44 |

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 683,887 sawa na asilimia 73.27 walichagua jibu sahihi A, *sikumkuta.* Hii inaonesha kwamba watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya sarufi, hususan katika matumizi ya lugha ambapo walielewa kuwa neno *sikumkuta* lina kiambishi kanushi ambacho ni si- na kiambishi kinachorejelea mtenda ambacho ni -ku- pamoja na kiambishi -m- kinachorejelea mtendwa hivyo kuweza kuleta upatanisho wa kisarufi kwenye swali husika.

Watahiniwa 249,436 sawa na asilimia 26.73 walichagua vipotoshi B *nilimkuta hayupo,* C *ninamkuta*, D *nitamkuta* na E *sitamkuta yupo.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi B *nilimkuta hayupo* hawakuelewa kuwa neno hilo halina upatanisho wa kisarufi na

halileti mantiki kwa sababu katika hali halisi huwezi kumkuta mtu halafu asiwepo. Uteuzi wa kipotoshi *ninamkuta* na *nitamkuta*, unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia wakati uliopita *"nilipokwenda kwake"* hivyo maneno *ninamkuta* au *nitamkuta* yapo katika wakati uliopo na ujao, badala ya wakati uliopita. Pia, uteuzi wa kipotoshi *sitamkuta yupo,* kauli hiyo haina mantiki wala upatanisho wa kisarufi kwa kuwa, nyakati mbili tofauti haziwezi kutumika kwa pamoja katika sentensi.

**Swali la 13:** Hapa _____________nilipokulia mimi. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A ndiyo


B ndimo

C ndipo

D ndiko

E ndicho

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kughamua upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mtawanyiko wa majibu na asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.




*Kielelezo Na. 3: Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 84.20 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi C, *ndipo* ambacho ni kitenzi kisaidizi chenye upatanisho wa kisarufi na kilichozingatia ngeli za nomino.

Asilimia 15.80 ya watahiniwa walichagua kipotoshi A *ndiyo,* B *ndimo,* D *ndiko na* E *ndicho.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ndiyo*, hawakuwa na uelewa kuwa neno hilo hutumika kama kitenzi kishirikishi au kisaidizi kutegemeana na muktadha wa sentensi. Hivyo, kwa mpangilio wa maneno katika sentensi kwenye swali hilo haiwezekani neno hilo liambatane na kitenzi kikuu "*nilipokulia.*" Uteuzi wa kipotoshi *ndimo*, neno ambalo hutumika kurejelea mahali ambapo ni ndani: hivyo kutokana na muundo wa sentensi katika swali, neno hilo halielezei mahali pa ndani, Uteuzi wa kipotoshi *ndiko*, kiambishi cha o –rejeshi kinachorejelea mahali mahususi ndani ya sehemu fulani aghalabu uteuzi wa kipotoshi *ndicho,*

watahiniwa hawakuelewa kuwa neno hilo ni kitenzi kishirikishi na wala si kiambishi cha o-rejeshi cha mahali. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini neno lenye kiambishi cha o-rejeshi “ndipo” ili kukamilisha sentensi hiyo.

**Swali la 14:** Baraka angelima kwa bidii angepata mavuno mengi. Sentensi hii ipo katika wakati gani?

A Uliopita

B Ujao

C Uliopo

D Timilifu

E Mazoea.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kutambua nyakati mbalimbali katika sentensi. Jedwali Na 11 linaonesha majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 11: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 736,434 | 53,859 | 60,069 | 48,342 | 31,209 | 3,410 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 78.90 | 5.77 | 6.44 | 5.18 | 3.34 | 0.37 |

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 736,434 sawa na asilimia 78.90 walichagua jibu sahihi A, *Uliopita*. Huu ni uthibitisho tosha kuwa, watahiniwa hao, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali jambo lililowawezesha kubaini kuwa sentensi hiyo ipo katika wakati uliopita.

Aidha, watahiniwa 196,889 sawa na asilimia 21.10 walichagua kipotoshi B *Ujao,* C *Uliopo,* D *Timilifu* na E *Mazoea.* Watahiniwa

waliochagua kipotoshi *Ujao,* hawakufahamu kuwa wakati “ujao” unatokana na kuwepo kiambishi -ta- katika kitenzi. Aidha, wakati *Uliopo*, hutokana na uwepo wa kiambishi –na- katika kitenzi. Uteuzi wa kipotoshi *Timilifu*, ulitokana na watahiniwa kutokufahamu kuwa, wakati timilifu unatokana na kuwepo kiambishi –me- na uteuzi wa kipotoshi *Mazoea,* ulitokana na watahiniwa kutokufahamu kuwa, hali ya mazoea hutokana na uwepo wa kiambishi –hu- katika kitenzi. Kwa ujumla, watahiniwa walioteua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya nyakati mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 15:** Mama anamnyonyesha mtoto. Kitenzi “anamnyonyesha” kipo katika wakati gani?

A Ujao

B Uliopita

C Timilifu

D Mazoea

E Uliopo.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua nyakati mbalimbali katika sentensi. Jedwali Na. 12 linaonesha majibu na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 12: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 27,512 | 35,954 | 95,810 | 52,572 | 718,747 | 2,728 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 2.95 | 3.85 | 10.27 | 5.63 | 77.01 | 0.29 |

Watahiniwa 718,747 sawa na asilimia 77.01 walichagua jibu sahihi E *Uliopo.* Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa

ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali mathalan waliweza kubaini kuwa katika kitenzi, kuna kiambishi awali–*na-* ambacho kinaoonesha tendo linavyofanyika.

Hata hivyo, watahiniwa 214,576 sawa na asilimia 22.99 walichagua vipotoshi: A *Ujao,* B *Uliopita,* C *Timilifu* na D *Mazoea.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *ujao,* hawakuelewa kuwa wakati ujao unatokana na kuwepo kwa kiambishi -ta- katika kitenzi, waliochagua kipotoshi *timilifu* hawakuelewa kuwa wakati timilifu unatokana na kuwepo kwa kiambishi -me- katika kitenzi, waliochagua kipotoshi *mazoea,* hawakuelewa kuwa neno hilo sio nyakati ila ni hali ya mazoea. Hii inathibitisha kuwa watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya nyakati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 16:** "Kama angeliimba vizuri____________zawadi." Ni muundo upi unakamilisha sentensi hii kwa usahihi?

A angalipewa

B angepewa

C angelipewa

D wangalipewa

E wangelipewa.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati katika sentensi shurutia. Jedwali Na.13 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 13: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 52,576 | 108,067 | 738,145 | 17,393 | 14,790 | 2,352 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.63 | 11.58 | 79.09 | 1.86 | 1.58 | 0.25 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 738,145 sawa na asilimia 79.09 waliweza kuchagua jibu sahihi C, *angelipewa.* Watahiniwa hao walielewa dhana ya sentensi shurutia kuwa ni sentensi za masharti ambazo huwa na pande mbili zinazotegemeana kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi.

Aidha, watahiniwa 195,178 sawa na asilimia 20.91 walichagua vipotoshi A *angalipewa,* B *angepewa* D wangalipewa na E *wangelipewa*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa kuhusu sentensi shurutia ambayo lazima ioneshe upatanisho wa kisarufi ambao una pande mbili katika sentensi, upande mmoja wa sentensi ukiwa na viambishi awali vya *angeli-* ni lazima upande wa pili wa swali nao uwe na viambishi hivyo vya awali na si vinginevyo.

**Swali la 17:** "Ninajifunza Hisabati kwa bidii." Sentensi hii iko katika kauli gani?

A Halisi


B Taarifa

C Ombi

D Hiari

E Amri.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kauli mbalimbali za vitenzi. Kielelezo Na. 4 linaonesha machaguo ya watahiniwa katika swali hili.




*Kielelezo Na. 4:Asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo.*

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 72.78 ya watahiniwa waliweza kubaini kwa usahihi kauli ya sentensi “Ninajifunza Hisabati kwa bidii” kuwa ni A, *Halisi*.

Hata hivyo, watahiniwa 254,056 sawa na asilimia 27.22 walichagua kipotoshi B *taarifa,* C *Ombi,* D *Hiari na* E *Amri*. Uteuzi wa kipotoshi *Taarifa* kina maana ya tungo inayotoa taarifa juu ya kitu, mtu, au jambo fulani. Uteuzi wa kipotoshi *ombi,* chenye maana ya maneno au ishara anayoitoa mtu kwa mtu mwingine mwenye uwezo wa kumsaidia, kipotoshi *hiari,* ni neno lenye maana ya uamuzi unaofikiwa na mtu bila kushurutishwa au ridhaa na kipotoshi amri, tungo zinazotoa rai, himizo au sihi kwa kitu fulani. Kwa ujumla,

uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu kauli mbalimbali zinavyotokea katika sentensi.

**Swali la 18** "Kandida hakupigwa na dada yake." Sentensi hii ipo katika hali gani?

A Ukanushi

B Uyakinishi

C Masharti

D Matarajio

E Mazoea.

Swali hili lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua hali mbalimbali katika sentensi za Kiswahili. Jedwali Na 14 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na 14 Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 735,389 | 35,017 | 39,896 | 50,237 | 67,754 | 5,030 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 78.79 | 3.75 | 4.27 | 5.38 | 7.26 | 0.54 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 735,389 sawa na asilimia 78.79 walichagua jibu sahihi A, *Ukanushi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa sentensi kanushi huundwa na kiambishi kanushi *ha-* katika kitenzi.

Hata hivyo, watahiniwa 197,934 sawa na asilimia 21.21 walichagua vipotoshi B *Uyakinishi,* C *Masharti, D Matarajio* na E *Mazoea.* Kipotoshi u*yakinishi,* ni sentensi zinazoelezea kitu au jambo fulani*.* Kipotoshi *masharti* humaanisha tungo zinazoelezea hali au shinikizo ili kitu fulani kitokee lazima kitu kingine kifanyike*,* kipotoshi *matarajio*, ni neno lenye maana ya kutazamia kupata kitu au kufanikisha jambo

na kipotoshi *mazoea* ni hali ya kurudia ufanyikaji wa tendo mara kwa mara. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa kuhusu hali mbalimbali zinazotokea katika sentensi.

**Swali la 19:** Wingi wa neno “yeye” ni upi?

A sisi
B nyinyi
C mimi
D wao
E wewe.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu nafsi mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na 15 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 15: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 114,459 | 259,544 | 46,568 | 464,364 | 44,352 | 4,036 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 12.26 | 27.81 | 4.99 | 49.75 | 4.75 | 0.43 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni cha wastani ambapo watahiniwa 464,364 sawa na asilimia 49.75 walichagua jibu sahihi D, *wao.* Jibu hili linathibitisha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nafsi mbalimbali hususani nafsi ya tatu na hivyo kubaini kwa usahihi kuwa neno “yeye” ni kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja na wingi wake ni *wao*.

Jumla ya watahiniwa 468,969 sawa na asilimia 50.25 walichagua vipotoshi A *sisi,* B *nyinyi,* C *mimi* na E *wewe*. Watahiniwa

waliochagua vipotoshi *sisi* na *mimi* hawakuwa na maarifa kuwa *mimi* ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja na wingi wake ni *sisi,* na uteuzi wa vipotoshi *nyinyi* na *wewe* unathibitisha kuwa hawakuelewa neno *wewe* ni kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja na *nyinyi* ni kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi, hivyo kushindwa kubaini wingi wa neno “yeye” ambao ni *wao*.

**Swali la 20:** Neno “soma” likibadilishwa na kuwa katika kauli ya kutendeka litakuwa neno lipi kati ya maneno yafuatayo?

A Someana

B Someshwa

C Somesha

D Someka

E Somwa.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kubaini kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na 16 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 16: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 47,476 | 79,027 | 63,631 | 66,0437 | 78,467 | 4,285 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.09 | 8.47 | 6.82 | 70.76 | 8.41 | 0.46 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 660,437 sawa na asilimia 70.76 walichagua jibu sahihi D, *Someka*. Watahiniwa hao waliweza kubaini tabia ya kitenzi kupokea viambishi tamati baada ya mzizi wa neno **som-** kwa

kupachika kiambishi *-ek-* katika kauli ya kutendeka na kupata neno "someka."

Watahiniwa 272,886 sawa na asilimia 29.24 walichagua kipotoshi A *Someana,* B *Someshwa,* C *Somesha na* E *Somwa.* Hii inaonesha kuwa watahiniwa waliochagua kipotoshi *someana,* hawakuelewa kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendeana, waliochagua kipotoshi *someshwa,* walishindwa kufahamu kuwa neno hilo lipo katika kauli ya kutendeshwa, waliochagua kipotoshi *somesha* hawakufahamu kuwa neno hilo ni kauli ya kutendesha na waliochagua kipotoshi *somwa* hawakufahamu kuwa ni kauli ya kutendwa. Kwa jumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu viambishi vya kauli mbalimbali katika lugha ya Kiswahili na hivyo, kushindwa kubaini kauli ya kutendeka –ek- katika neno *someka*.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) ambayo yalimtaka mtahiniwa kutambua matumizi ya lugha ya kifasihi katika methali, nahau, misemo na vitendawili, hususan, katika kuelewa maana, miundo na matumizi yake katika lugha ya Kiswahili.

**Swali la 21:** "Mwenzako akinyolewa _____________." Kifungu kipi cha maneno kinakamilisha methali hii?

A wewe tazama pembeni

B wewe ondoka

C zako tia maji

D subiri zamu yako

E zako nyoa.

Swali hili lilikuwa na lengo la kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua muundo na maana ya methali za Kiswahili. Jedwali Na. 17 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 17: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 20,338 | 20,509 | 834,112 | 40,209 | 15,419 | 2,736 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 2.18 | 2.20 | 89.37 | 4.31 | 1.65 | 0.29 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 834,112 sawa na asilimia 89.37 waliweza kukamilisha methali kwa kuchagua jibu sahihi C, *zako tia maji*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa methali husika na kwamba methali huundwa na pande mbili zinazotegemeana kidhima na kimaana.

Aidha, watahiniwa 99,211 sawa na asilimia 10.63 walichagua vipotoshi A *wewe tazama pembeni*, B *wewe ondoka*, D *subiri zamu yako* na E *zako nyoa*. Uteuzi wa vipotoshi *wewe tazama pembeni* na *wewe ondoka* ulitokana na watahiniwa kuhusisha dhana hiyo na hali ya kumkataza mtu kutokuwepo mahali anaponyolewa mtu mwingine kama jambo lisilofaa/baya wakihusisha kimakosa na *zako tia maji*; kauli iliyotakiwa kukamilisha methali hii.

Hata hivyo, watahiniwa waliochagua kipotoshi *subiri zamu yako* na *zako nyoa* walivutiwa na dhana kuwa, umwonapo mtu akinyolewa sharti nawe unyolewe wakiihusisha kimakosa na kauli *zako tia maji* inayokamilisha methali husika kwa usahihi. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na

weledi wa kutosha kuhusu miundo ya methali na hivyo kushindwa kukamilisha methali kulingana na matakwa ya swali.

**Swali la 22:** "Vita vya panzi furaha ya kunguru." Methali hii ina maana ipi kati ya zifuatazo?

A Panzi wakipigana kunguru nao hupigana

B Marafiki wakigombana ni furaha kwa maadui

C Kunguru anawagombanisha panzi

D Marafiki wakiwa wengi ni lazima wagombane

E Panzi wanapigana vita mara kwa mara.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana za methali za Kiswahili. Jedwali Na. 18 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 18: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 27,240 | 800,736 | 30,711 | 47,025 | 23,871 | 3,740 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 2.92 | 85.79 | 3.29 | 5.04 | 2.56 | 0.40 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 800,736 sawa na asilimia 85.79 walichagua jibu sahihi B *Marafiki wakigombana ni furaha kwa maadui*. Matumizi ya methali hiyo ni kuwa, watu wawili ambao ni jamaa/marafiki wanapogombana humfaidisha mtu wa tatu/asiyehusika (adui). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya maana za methali husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 132,587 sawa na asilimia 14.21 walichagua vipotoshi A *Panzi wakipigana kunguru nao hupigana*, C *Kunguru anawagombanisha panzi*, D *Marafiki wakiwa wengi ni lazima wagombane na* E *Panzi wanapigana vita mara kwa mara*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa kuhusu maana ya methali “Vita vya panzi furaha ya kunguru” badala yake walichagua maana ambazo ni tofauti na jibu sahihi la swali. Kwa mfano, kipotoshi *panzi wakipigana kunguru nao hupigana*, *kunguru anawagombanisha panzi na panzi wanapigana vita mara kwa mara*, waliangalia maana yake katika umbo la nje (maana ya moja kwa moja) kuwa, panzi hugombana/kupigana kila mara na kunguru husababisha panzi kugombana. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *marafiki wakiwa wengi ni lazima wagombane* walizingatia maana ya nje kuwa, marafiki wanapokuwa wengi kugombana hakuzuiliki.

**Swali la 23:** “Usipoziba ufa utajenga ukuta.” Methali ipi kati ya methali zifuatazo ina maana sawa na methali hii?

A Asiyekuwepo na lake halipo

B Mdharau mwiba mguu huota tende

C Haba na haba hujaza kibaba

D Kata pua uunge wajihi

E Usiache mbachao kwa msala upitao.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya methali za Kiswahili. Jedwali Na. 19 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na.19: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 69,323 | 562,783 | 69,308 | 63,590 | 161,746 | 6,573 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.43 | 60.30 | 7.43 | 6.81 | 17.33 | 0.70 |

Watahiniwa 562,783 sawa na asilimia 60.30 waliweza kuchagua jibu sahihi B *Mdharau mwiba mguu huota tende* kwa kuwa walikuwa na maarifa kuhusu methali zenye maana sawa kimatumizi. Methali hii ina maana kuwa, tusidharau jambo fulani linapoanza kwenda vibaya badala yake tufanye juhudi za kutengeneza la sivyo tutapata madhara makubwa sawa na methali isemayo "*usipoziba ufa utajenga ukuta*."

Watahiniwa 370,540 sawa na asilimia 39.70 walichagua vipotoshi A *Asiyekuwepo na lake halipo,* C *Haba na haba hujaza kibaba,* D *Kata pua uunge wajihi* na E *Usiache mbachao kwa msala upitao*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *asiyekuwepo na lake halipo* ikimaanisha kuwa, mtu asiyekuwapo mahali fulani husahaulika na kuhusisha kimakosa na methali "usipoziba ufa utajenga ukuta" ambayo maana yake ni kutodharau mambo madogo bali hupaswa kushughulikiwa mapema ili yasije yakawa makubwa.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *haba na haba hujaza kibaba*, ikiwa na maana ya kuweka vitu vidogo vidogo ili kupata vingi hawakuelewa kuwa maana ya methali hiyo siyo sawa na methali "usipoziba ufa utajenga ukuta." Uteuzi wa kipotoshi *kata pua uunge wajihi* ikiwa na maana ya jambo linaloonekana kuwa baya/gumu mwishowe huleta manufaa makubwa na kipotoshi *usiache mbachao kwa msala upitao* yenye maana ya kutodharau

vitu vya zamani vinavyofaa baada ya kupata vipya; walishindwa kuelewa maana ya methali hizo kuwa hazina uhusiano kabisa na methali, “Usipoziba ufa utajenga ukuta.”

**Swali la 24**: “Kila mtu humwabudu apitapo.” Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Mzazi

B Polisi

C Mlango

D Kanisa

E Msikiti.

Swali hili lilikuwa linapima ujuzi wa mtahiniwa kutegua vitendawili. Jedwali Na. 20 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 20: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 21,615 | 26,779 | 833,557 | 30,225 | 18,122 | 3,025 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 2.32 | 2.87 | 89.31 | 3.24 | 1.94 | 0.32 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 833,557 sawa na asilimia 89.31 walichagua jibu sahihi C *Mlango* ambalo linategua kitendawili husika. Hii inathibitisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya fumbo lililojenga katika kitendawili hicho.

Watahiniwa 99,766 sawa na asilimia 10.69 walichagua kipotoshi A *Mzazi,* B *Polisi,* D *Kanisa* na E *Msikiti* kwa kukosa maarifa ya udadisi katika vipotoshi hivyo, hatimaye kushindwa kutegua

kitendawili husika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mzazi* walikuwa na dhana isiyo sahihi kwamba, kwa kuwa mzazi ni muhimu na hustahili kuheshimiwa wakati wote, hivyo kulinganisha na kitendawili "Kila mtu humwabudu apitapo." Watahiniwa waliochagua kipotoshi *polisi* yaani watu waliofunzwa na kupewa dhamana ya kudumisha amani na kuhakikisha utekelezaji wa kisheria ambapo jamii hupaswa kuheshimu na wala siyo kuabudu, waliochagua kipotoshi *kanisa* na *msikiti ambamo* watu humwabudu Mungu siku zote na sio mahali pa kupita kama ilivyo *mlango*. Hivyo watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kufumbua mafumbo yaliyojengwa katika vitendawili hatimaye kushindwa kutegua kitendawili "Kila mtu humwabudu apitapo."

**Swali la 25:** "Anajihami bila silaha." Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A Nungunungu


B Mbwa

C Kinyonga

D Mbogo

E Paka.

Swali hili lilipima ujuzi wa mtahiniwa wa kutegua vitendawili. Kielelezo Na. 5 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo




Kielelezo Na. 5 kinaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 85.75 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi C *Kinyonga*. Watahiniwa hao, walifahamu kuwa kinyonga ana tabia ya kujikinga na maadui zake kwa kubadili rangi yake kufuatana na mazingira aliyopo.

Watahiniwa 132,964 sawa na asilimia 14.25 walichagua kipotoshi A *Nungunungu,* B *Mbwa,* D *Mbogo* na E *Paka* kwa kukosa maarifa ya udadisi katika vipotoshi hivyo, hatimaye kushindwa kutegua kitendawili husika. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nungunungu* walikuwa na dhana isiyo sahihi kuwa nungunungu hujihami kwa kurusha miba yake kwa adui ili kuwa salama na hivyo kulinganisha na kitendawili "Anajihami bila silaha."

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mbwa* ambao huhusika na ulinzi na usalama wa mali za watu huweza kujihami kwa kung'ata adui ili wasidhurike, kipotoshi *mbogo* ni mnyama mkubwa wa porini mwenye pembe kubwa zilizokunjika mbele ili kujihami na maadui

na kipotoshi *paka* ni mnyama wakufugwa na hodari kwa kuwinda na kula panya anayejihami na adui kwa kutumia kucha. Hivyo, uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kufumbua mafumbo yaliyojengwa katika vitendawili hatimaye kushindwa kutegua kitendawili “Anajihami bila silaha.”

**Swali la 26:** “Huku fungu huku fungu katikati bahari.” Kitendawili hiki kina maana gani?

A Firigisi

B Kiazi

C Meli

D Nazi

E Mtumbwi.

Swali hili lilikuwa linapima ujuzi wa watahiniwa katika kutegua vitendawili. Jedwali Na. 21 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 21: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 158,379 | 59,277 | 63,256 | 563,419 | 82,005 | 6,987 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.97 | 6.35 | 6.78 | 60.37 | 8.79 | 0.75 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 563,419 sawa na asilimia 60.37 walichagua jibu sahihi D *Nazi* ambayo ni tunda la mnazi lililo ndani ya kifuu kilichozingirwa na kumbi lenye nyama nyeupe na maji katikati. Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya fumbo lililojengwa katika kitendawili hivyo kutegua kwa usahihi kuwa ni *nazi*.

Watahiniwa 369,904 sawa na asilimia 39.63 walichagua kipotoshi A *Firigisi,* B *Kiazi,* C *Meli* na E *Mtumbwi* kwa kukosa maarifa ya udadisi katika vipotoshi hivyo visivyo na uhusiano na kitendawili "Huku fungu huku fungu katikati bahari" hivyo kushindwa kutegua kitendawili hicho. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *firigisi* ambayo ni kiungo cha ndani ya tumbo la ndege kinachotumika kusaga chakula. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *kiazi ambacho ni mmea unaotambaa ambao mizizi yake huliwa*, *meli* chombo kikubwa cha baharini kinachotengenezwa kwa metali kwa ajili ya kusafirisha watu na mizigo na *mtumbwi* chombo kinachotengenezwa kwa gogo na kinachosafirisha watu kwenye maji na kuvulia samaki. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakufahamu kuwa maumbo ya vitu vilivyotajwa hayasadifu umbo lililofichwa katika kitendawili husika.

**Swali la 27:** “Kaa chonjo.” Nahau hii maana yake ni ipi?

A Kaa pembeni

B Kuwa mwangalifu

C Kuwa mwaminifu

D Kuwa mcheshi

E Kuwa mjanja.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua maana ya semi za Kiswahili. Jedwali Na. 22 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 22: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 216,591 | 594,692 | 34,311 | 27,294 | 57,061 | 3,374 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 23.21 | 63.72 | 3.68 | 2.92 | 6.11 | 0.36 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 594,692 sawa na asilimia 63.72 walichagua chaguo sahihi B *Kuwa mwangalifu.* Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa wanafahamu kuwa "Kaa chonjo" ni kumpa mtu tahadhari katika utendaji wa jambo fulani ili kuepuka madhara yake.

Watahiniwa 338,631 sawa na asilimia 36.30 walichagua vipotoshi A *Kaa pembeni*, C *Kuwa mwaminifu*, D *Kuwa mcheshi* na E *Kuwa mjanja.* Hii inaonesha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubaini dhana ya nahau "Kaa chonjo" badala yake walichagua majibu yasiyo sahihi ambapo walichagua kipotoshi *Kaa pembeni* kauli yenye maana ya kuwa mbali wakati jambo fulani linapotendeka ambapo haina uhusiano na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi *Kuwa mwaminifu*, kauli yenye maana ya hali ya kuishi sawasawa na maadili ya Mungu, jamii au sheria fulani. Vilevile, baadhi ya watahiniwa walichagua vipotoshi *Kuwa mcheshi* na *Kuwa mjanja* kauli zenye maana ya hali ya kuchangamkia na kuwa na ufahamu wa jambo vilivyo, majibu ambayo hayakidhi matakwa ya swali.

Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu semi za lugha ya Kiswahili hususan nahau ambazo kimsingi hutumia maneno ya

kawaida yaliyobeba maana iliyojificha. Kwa mfano, neno "chonjo" lina maana ya tunda linalotoa maji ya mnato" lakini huwasilisha maana ya *uangalifu*.

**Swali la 28:** “Alipomwona simba alipigwa na butwaa.” Maneno “alipigwa na butwaa” maana yake nini?

A Alizimia


B Alikufa

C Alikimbia

D Alidondoka

E Alishangaa.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutoa maana na matumizi ya misemo. Kielelezo Na. 6 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo Na. 6*: Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo.*

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri ambapo watahiniwa 786,234 sawa na asilimia 84.24 walichagua jibu sahihi E *Alishangaa* ambayo maana yake ni kustaajabu/kupumbaa kwa kuona jambo la ajabu. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msemo "alipigwa na butwaa" na kuweza kuihusisha na hali ya *kumwona simba na kushangaa*.

Aidha, watahiniwa 147,089 sawa na asilimia 15.80 walichagua kipotoshi A *Alizimia*, B *Alikufa*, C *Alikimbia* na D *Alidondoka*. Watahiniwa hao, walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani waliandika majibu ambayo yanarejea mwitiko baada ya kumwona simba badala ya maana ya msemo "alipigwa butwaa".

**Swali la 29:** "Walimu walimshauri mwanafunzi amwangukie baba yake." Neno "amwangukie" lina maana gani?

A Amwokoe

B Amtake radhi

C Amtulize

D Amtimizie mahitaji

E Amtunze.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya misemo. Jedwali Na. 23 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 23: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 78,534 | 678,116 | 35,585 | 80,241 | 56,431 | 4,416 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.41 | 72.66 | 3.81 | 8.60 | 6.05 | 0.47 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili ni kizuri ambapo watahiniwa 678,116 sawa na asilimia 72.66 walichagua jibu sahihi B *Amtake radhi* yenye maana ya kuomba msamaha kwa kosa fulani. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya msemo "amwangukie" na kuweza kuhusisha na hali ya mwanafunzi kushauriwa na walimu *kuomba msamaha* kwa baba yake baaada ya kukosa.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 255,207 sawa na asilimia 27.34 walichagua vipotoshi A *Amwokoe,* C *Amtulize,* D *Amtimizie mahitaji* na E *Amtunze.* Uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kuhusianisha maneno: amwokoe, amtulize, amtimizie mahitaji na amtunze na wajibu wa watoto kwa wazazi wao hivyo kushindwa kubaini jibu sahihi "amtake radhi"

**Swali la 30:** Wanakijiji walifanya kazi bega kwa bega. Usemi "bega kwa bega" una maana gani?

A Ushirikiano

B Utengano

C Ubaguzi

D Umaridadi

E Uzoefu.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya semi mbalimbali. Jedwali Na. 24 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 24: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 85,9876 | 24,139 | 18,333 | 14,899 | 12,862 | 3,214 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 92.13 | 2.59 | 1.96 | 1.60 | 1.38 | 0.34 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri zaidi katika swali hili ambapo watahiniwa 859,876 sawa na asilimia 92.13 waliweza kubaini maana ya usemi kwa kuchagua jibu sahihi A *Ushirikiano* jambo linaloonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya usemi "bega kwa bega" ambao huimiza watu kuwa na *ushirikiano* katika kazi ili kuleta maendeleo ya pamoja.

Hata hivyo, watahiniwa 73,447 sawa na asilimia 7.87 walichagua vipotoshi B *Utengano,* C *Ubaguzi,* D Umaridadi *na E uzoefu,* kutokana na kukosa uelewa wa maana ya usemi husika*.* Watahiniwa hao waliochagua kimakosa kipotoshi *utengano* lenye maana kinyume cha usemi "bega kwa bega", kipotoshi ubaguzi, kutoa huduma bila usawa, umaridadi, muonekano wa kupendeza wa watu/ kitu au sehemu, na uzoefu, ufanyaji wa kitu au jambo kwa muda mrefu unaojenga mazoea, majibu ambayo siyo matakwa ya swali.

## 2.3 Sehemu C: Ushairi

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita (6) ambayo yalimtaka mtahiniwa kusoma kwa makini shairi na kutumia maarifa aliyojifunza katika ushairi kujibu maswali yaliyotokana na shairi hilo. Watahiniwa walipewa shairi lifuatalo:

Kiswahili lugha pana, wote tunaifahamu,
Kina uwanja mpana, jirani wapata hamu,
Uhuru tulipigana, na Nyerere afahamu,
Kiswahili lugha yetu, Tanzania twaringia.

Elimu kufundishia, ujumbe kufikishia,
Na wanazuoni pia, Kiswahili kutetea,

TATAKI hajabakia, na lugha kutukuzia,
Kiswahili lugha yetu, Tanzania twaringia.

Na wasomi watetea, Kiswahili kutumika,
Masomo kufundishia, ni muhimu kutumika,
Hata vijijini pia, Kiswahili chasifika,
Kiswahili lugha yetu, Tanzania twaringia.

Wote kinatuauni, usitake leta gubu,
Shuleni tujadilini, tusiwe kama mabubu,
Mwasisi tumsifuni, ajizi hakujaribu,
Kiswahili lugha yetu, Tanzania twaringia.

**Swali la 31:** Kichwa kinachofaa kwa shairi hili ni kipi?

A Elimu yetu


B Lugha na majirani

C Wasomi na wanakijiji

D Lugha ya Kiswahili

E Kumsifu Mwalimu Nyerere.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua kichwa cha shairi alilolisoma. Kielelezo Na. 7 kinaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa katika kila chaguo.




Kielelezo Na. 7: *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo*

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 82.14 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi D *Lugha ya Kiswahili.* Hii inaonesha kwamba watahiniwa waliochagua jibu hilo walitambua mawazo makuu ambayo yanajirudia katika kila ubeti wa shairi kutokana na umakini katika usomaji hivyo kubaini kichwa cha shairi hilo kwa usahihi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 166,735 sawa na asilimia 17.86 walichagua vipotoshi A *Elimu yetu,* B *Lugha na majirani,* C *Wasomi na wanakijiji* na E *Kumsifu Mwalimu Nyerere.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *elimu yetu* walivutiwa na ubeti wa pili kuwa lugha hutumika katika kutolea elimu ambalo siyo jibu sahihi kwani shairi linahimiza umuhimu wa Lugha ya Kiswahili. Uchaguzi wa kipotoshi *lugha na majirani,* ulisababishwa na watahiniwa kuona

kuwa lugha huweza kutumika na watu kutoka nje ya eneo fulani linalotumia lugha husika.

Aidha, uteuzi wa kipotoshi *wasomi na wanakijiji* ulitokana na watahiniwa kuhusisha ujumbe uliopo katika ubeti wa tatu na matumizi ya lugha kwa wasomi na wanakijiji. Hata hivyo, uchaguzi wa kipotoshi *kumsifu Mwalimu Nyerere* ulitokana na watahiniwa hao kuhusisha juhudi za Mwalimu Nyerere za kupigania uhuru na wazo kuu la shairi. Kwa jumla, uteuzi wa vipotoshi hivyo hauendani na kichwa cha shairi kwani baadhi ya maneno hayo yalijitokeza katika sehemu chache za shairi.

**Swali la 32:** Vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa nne ni vipi?

A ni na bu

B tu na a

C ni na u

D ni na tu

E ni na a.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 25 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 25: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 723,268 | 67,455 | 71,459 | 40,160 | 26,604 | 4,377 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 77.49 | 7.23 | 7.66 | 4.30 | 2.85 | 0.47 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 723,268 sawa na asilimia 77.49 waliweza kuchagua jibu sahihi A *ni* na *bu* ambazo ni silabi za mwisho katika kila kipande cha ubeti wa nne wa shairi hilo. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi, hivyo kubaini vina vya kati na vya mwisho katika ubeti husika kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 210,055 sawa na asilimia 22.51 walichagua vipotoshi B *tu* na *a,* C *ni* na *u,* D *ni* na *tu,* E *ni* na *a.* Watahiniwa hao walikosa maarifa juu ya dhana ya vina katika shairi kwani walichagua silabi ambazo zimetokea katika shairi kwenye nafasi ambazo haziwezi kuwa na sifa ya vina vya kati wala vya mwisho kwa mujibu wa kanuni za muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na uchaguzi wa vipotoshi hivyo, inathibitisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vina vya kati na mwisho katika ubeti wa shairi.

**Swali la 33:** Mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi huitwaje?

A Mizani

B Vina

C Hitimisho

D Mshororo

E Kituo.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi. Jedwali Na. 26 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 26: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 38,263 | 46,457 | 73,714 | 205,189 | 563,721 | 5,979 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 4.10 | 4.98 | 7.90 | 21.98 | 60.40 | 0.64 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 563,721 sawa na asilimia 60.40 walichagua jibu sahihi E *Kituo.* Huu ni uthibitisho kwamba watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha hivyo, waliweza kubaini kuwa *kituo* ni mstari wa mwisho katika kila ubeti ambao huonesha kiini au msisitizo katika ubeti wa shairi.

Aidha, watahiniwa 369,602 sawa na asilimia 39.60 walishindwa kutaja jina linalotumika katika mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi kwa kukosa maarifa ya kubaini kiini/msisitizo katika ubeti wa shairi, hivyo walichagua vipotoshi A *Mizani,* B *Vina,* C *Hitimisho na* D *Mshororo.* Watahiniwa waliochagua kipotoshi *mizani* hawakuelewa kuwa, neno hilo halitokani na mstari wa mwisho wa shairi unaonesha msisitizo katika ubeti wa shairi bali ni jumla ya silabi katika mshororo wa shairi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *Vina*, walihusisha kimakosa silabi ya kati na mwisho katika mstari wa kila ubeti na ujumbe uliopo katika mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *hitimisho,* walifananisha neno hilo kimakosa na ujumbe unaopatikana katika mstari wa mwisho wa shairi badala ya kiini/msisitizo wa ubeti wa shairi. Vilevile, waliochagua kipotoshi *mshororo,* walishindwa kuzingatia maana ya neno hilo kuwa ni mstari wowote katika ubeti wa shairi badala ya kuzingatia mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi kulingana na matakwa ya swali. Hivyo, watahiniwa waliochagua

vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu "kituo" ambayo ni mstari wa mwisho wa ubeti wa ushairi.

**Swali la 34**: Shairi hili lina mizani ngapi?

A. Nane
B. Kumi na sita
C. Nne
D. Kumi na mbili
E. Kumi na nne.

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu muundo wa shairi katika lugha ya Kiswahili. Jedwali Na. 27 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 27: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 34,000 | 788,826 | 66,842 | 23,195 | 16,065 | 4,395 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 3.64 | 84.52 | 7.16 | 2.49 | 1.72 | 0.47 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kizuri, kwani jumla ya watahiniwa 788,826 sawa na asilimia 84.52 waliweza kuchagua jibu sahihi *B kumi na sita*. Watahiniwa hao walifahamu kuwa mizani ni jumla ya silabi katika mshororo (mstari) wa shairi.

Hata hivyo, watahiniwa 144,497 (15.48%) walichagua vipotoshi A Nane, C Nne, D Kumi na mbili na E Kumi na nne kwa kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu mizani katika mashairi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nane*, walihusisha na idadi ya silabi katika kipande kimoja cha mstari badala ya kutaja idadi ya mizani kwa mstari mzima.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *nne*, walihesabu idadi ya mistari katika ubeti, kipotoshi *kumi na mbili* hawakuwa na maarifa kuhusu mizani na waliochagua kipotoshi *kumi na nne*, walihesabu idadi ya maneno katika mistari mitatu ya mwanzo ya ubeti husika badala ya kuhesabu silabi katika kila mstari yaani mizani. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muundo wa shairi hususan katika dhana ya mizani.

**Swali la 35:** Neno "gubu" kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?

A Vita

B Ghasia

C Amana

D Umaskini

E Anasa.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya msamiati uliotumika katika shairi. Jedwali Na. 28 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 28: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 233,857 | 446,249 | 74,905 | 91,967 | 80,159 | 6,186 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.06 | 47.81 | 8.03 | 9.85 | 8.59 | 0.66 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 446,249 sawa na asilimia 47.81 waliweza kuchagua jibu B *Ghasia* ikiwa na maana ya tukio la vurugu na fujo linalosababisha kutokuwepo kwa hali ya amani. Watahiniwa hao waliweza

kuhusianisha msamiati *gubu* na neno *ghasia* ambalo linabeba maana ya msingi ya msamiati huo kama lilivyotumika katika shairi.

Aidha, watahiniwa 487,074 sawa na asilimia 52.19 walichagua vipotoshi A *Vita,* C *Amana,* D *Umaskini* na E *Anasa* kutokana na kukosa maarifa ya kubaini maana ya neno kama lilivyotumika katika shairi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *vita* hawakuelewa kuwa maana ya neno hilo ni mapambano/mapigano baina ya watu au wanyama ambayo inakinzana na maana ya *gubu.*

Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *amana,* hawakutambua kuwa, neno hilo huonesha kitu anachokabidhiwa mtu kukihifadhi kwa muda ili akirejeshe baadaye, uteuzi wa kipotoshi *umaskini* ulitokana na watahiniwa kutokuelewa kuwa ni hali duni ya kimaisha inayoweza kumkuta mtu/shirika/nchi kutokuwa na mali na waliochagua kipotoshi *anasa* hawakuelewa kuwa ni hali ya raha na starehe. Hivyo, kutokana na maana za vipotoshi hivyo inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa yakutosha kubaini maana ya msamiati “gubu” ambao unamaanisha *tabia ya kuudhi na usumbufu wa mara kwa mara au ugomvi* kama ulivyotumika katika shairi.

**Swali la 36:** Nini maana ya neno “wanazuoni” kama lilivyotumika katika shairi hili?

A Waliokwenda shule

B Waliosoma vitabu vingi

C Waliosoma masomo mengi

D Wanaojua kusoma na kuandika

E Wenye kubobea katika somo Fulani.

Swali hili lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutambua maana ya msamiati kama ulivyotumika katika shairi. Jedwali Na. 29 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 29: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 278,014 | 99,959 | 100,441 | 149,580 | 297,813 | 7,516 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 29.79 | 10.71 | 10.76 | 16.03 | 31.91 | 0.81 |

Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 635,510 sawa na asilimia 68.10 walichagua vipotoshi A *Waliokwenda shule*, B *Waliosoma vitabu vingi*, C *Waliosoma masomo mengi* na D *Wanaojua kusoma na kuandika.* Huu ni ni uthibitisho kuwa, watahiniwa hawakufahamu kuwa neno “wanazuoni” ni watu *wenye kubobea katika somo/fani fulani*.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 297,813 sawa na asilimia 31.90 waliweza kuchagua jibu sahihi E *Wenye kubobea katika somo fulani*. Watahiniwa hao, waliweza kuhusianisha msamiati *wanazuoni* na ufafanuzi “*wenye kubobea katika somo fulani”* ukiwa na maana ya watu mwenye utaalam au ujuzi wa hali ya juu katika fani fulani kama matokeo ya kuwa na kiwango cha juu cha elimu.

## 2.4 Sehemu D: Utungaji

Sehemu hii ililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Katika sehemu hii watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa

bila mtiririko sahihi na walitakiwa kuzipanga ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

37. Lilikuwa ni jukumu la kila jamii kuhakikisha kizazi kipya kinajua mila na desturi zao.

38. Hivyo, kila jamii ilikuwa na mfumo wa elimu unaoeleweka kabla ya ujio wa wageni nchini Tanzania.

39. Tangu zamani za mababu zetu watoto walikuwa wakipewa mafunzo mbalimbali ili kuwaandaa kwa kazi za utu uzima.

40. Watoto hao walifunzwa mila za wazazi wao, lugha, imani na kazi zilizofanywa na watu wa jamii ile.

**Swali la 37:** Lilikuwa ni jukumu la kila jamii kuhakikisha kizazi kipya kinajua mila na desturi zao.

Watahiniwa walitakiwa kupanga sentensi namba 37 kuwa sentensi ya tatu katika mtiririko unaoleta mantiki kwa kuandika herufi C. Jedwali Na. 30 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 30: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 49,711 | 164,840 | 440,394 | 261,998 | 12,917 | 3,463 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.33 | 17.66 | 47.19 | 28.07 | 1.38 | 0.37 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 440,394 sawa na asilimia 47.19 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi C ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Upangaji huu unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kubainisha sentensi hiyo kuwa ni ya tatu katika mtiririko wa habari hiyo kuhusu malengo ya elimu ya jadi. Hata hivyo, watahiniwa 12,917 sawa na asilimia 1.38 walichagua E isiyokuwa

na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi wa kutunga habari fupi yenye mantiki.

**Swali la 38:** Hivyo, kila jamii ilikuwa na mfumo wa elimu unaoeleweka kabla ya ujio wa wageni nchini Tanzania.

Watahiniwa walitakiwa kupanga sentensi namba 38 kuwa sentensi ya nne katika mtiririko unaoleta mantiki kwa kuandika herufi D. Jedwali Na. 31 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 31: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 46,313 | 115,163 | 260,072 | 495,191 | 13,027 | 3,557 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 4.96 | 12.34 | 27.87 | 53.06 | 1.40 | 0.38 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 495,191 sawa na asilimia 53.06 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi D ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Upangaji huu unaonesha kuwa, watahiniwa hao waliweza kubainisha sentensi hiyo kuwa ni ya nne katika mtiririko wa habari hiyo kuhusu uwepo wa elimu ya jadi kabla ya elimu ya kikoloni. Hata hivyo, watahiniwa 13,027 sawa na asilimia 1.4 walichagua E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi wa kutunga habari fupi yenye mantiki.

**Swali la 39:** Tangu zamani za mababu zetu watoto walikuwa wakipewa mafunzo mbalimbali ili kuwaandaa kwa kazi za utu uzima.

Watahiniwa walitakiwa kupanga sentensi namba 39 kuwa sentensi ya kwanza katika mtiririko unaoleta mantiki kwa kuandika herufi A. Jedwali Na. 32 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 32: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 767,007 | 63,842 | 47,367 | 42,384 | 9,725 | 2,998 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 82.18 | 6.84 | 5.08 | 4.54 | 1.04 | 0.32 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 767,007 sawa na asilimia 82.18 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi A ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Upangaji huu unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kubainisha sentensi hiyo kuwa ni ya kwanza katika mtiririko wa habari hiyo kuhusu mababu zetu walivyowaandaa watoto katika kazi za utu uzima. Hata hivyo, watahiniwa 9,725 sawa na asilimia 1.04 walichagua herufi E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi wa kutunga habari fupi yenye mantiki.

**Swali la 40:** Watoto hao walifunzwa mila za wazazi wao, lugha, imani na kazi zilizofanywa na watu wa jamii ile.

Watahiniwa walitakiwa kupanga sentensi namba 40 kuwa sentensi ya pili katika mtiririko unaoleta mantiki kwa kuandika herufi B. Jedwali Na. 33 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa kwa kila chaguo.

**Jedwali Na. 33: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 58,527 | 588,277 | 173,234 | 97,461 | 13,259 | 2,565 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 6.27 | 63.03 | 18.56 | 10.44 | 1.42 | 0.27 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 588,277 sawa na asilimia 63.03 walipanga sentensi hii katika mtiririko kwa kuandika kwa usahihi herufi B ili kuunda habari fupi yenye mantiki. Upangaji huu unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kubainisha sentensi hiyo kuwa ni ya kwanza katika

mtiririko wa habari hiyo kuhusu mababu zetu walivyowaandaa watoto katika kazi za utu uzima. Hata hivyo, watahiniwa 9,725 sawa na asilimia 1.04 walichagua herufi E isiyokuwa na sentensi yoyote kati ya sentensi zilizokuwa katika habari kutokana na kukosa ujuzi katika kutunga habari fupi zenye mantiki.

## 2.5 Sehemu E: Ufahamu

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano yaliyohusu ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia maarifa na ueledi katika kusoma kwa makini na kuelewa kifungu cha habari kisha kujibu maswali kutokana na habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa watahiniwa.

> Wasanii wana mchango mkubwa katika kufundisha jamii ya Watanzania. Watu hawa ukiwaona wanacheza, ukiwasikiliza wanavyoimba na kughani mashairi mwenyewe utawapenda. Wanaichambua jamii kwa namna mbalimbali. Kusema kweli ni watu wanaoonesha umuhimu wao kwa jamii nzima ya Watanzania. Viongozi wengi kama sio wote wanatumia wasanii hawa kuhamasisha watu waje kuwasikiliza kwenye mikutano yao.
>
> Wasanii wanasimama na kuitukuza nchi yetu. Wanaeleza umuhimu kwa wananchi kuitunza amani iliyopo nchini, utajiri wa nchi yetu yakiwemo madini, wanyama, milima ukiwemo mlima Kilimanjaro pamoja na maziwa na mito mbalimbali.
>
> Wasanii hawa wanachukizwa sana na ufisadi pamoja na wizi unaofanywa na baadhi ya wanajamii kwa tamaa ya kujilimbikizia mali huku wananchi wakibaki katika hali duni ya maisha. Wanafichua maovu mbalimbali ya wanajamii kupitia sanaa.
>
> Watanzania kwa pamoja tuwaenzi wasanii hawa na tuachane na tabia ya kuthamini wasanii wa kigeni. Wasanii wetu wanatuelimisha mambo mbalimbali yanayohusu jamii yetu.

**Swali la 41:** Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?


Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa ufahamu. Jedwali Na. 34 linaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 41.

**Jedwali Na. 34 Idadi na Asilimia ya Watahiniwa kwa kila Alama**

| **Alama** | **0.0** | **0.5** | **1.0** | **1.5** | **2.0** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 192,155 | 10,588 | 132,912 | 10,766 | 586,909 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.59 | 1.13 | 14.24 | 1.15 | 62.88 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 730,587 sawa na asilimia 78.28 walijibu swali hili vizuri.

Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha katika kusoma habari waliyopewa na hivyo kuandika kwa usahihi kichwa cha habari. Watahiniwa hao walionesha kuwa na wigo mpana wa majibu yao kutokana na kuelewa vyema kiini cha habari hiyo, hivyo waliandika kichwa cha habari kwa kutumia maneno/kauli zilizotumika katika habari kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kichwa cha habari “Mchango wa Wasanii” na kupata alama zote. Kielelezo Na. 8 kinaonesha jibu zuri la mtahiniwa huyo.



41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?

Mchango wa wasanii

*Kielelezo Na*. 8: Kichwa sahihi cha *kifungu cha habari.*

Aidha, watahiniwa 202,743 sawa na asilimia 21.72 walishindwa kubaini kichwa cha habari kutokana na kutoelewa habari husika. Watahiniwa hao walikosa umakini katika usomaji wa habari hivyo kushindwa kubaini mawazo makuu yaliyomo kwenye habari kama


vile: umuhimu wa wasanii, wasanii, kuwaenzi wasanii, wasanii wa Tanzania, thamani ya wasanii na mchango wa wasanii kwa jumla. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa jibu nje ya habari aliyoisoma kwa kuandika "Nomino" neno ambalo hutaja jina la mtu/vitu au mahali na ni miongoni mwa aina za maneno ya Kiswahili, hivyo kukosa uhusiano na kifungu cha habari. Kielelezo Na 9 ni mfano wa jibu la mtahiniwa huyo.


41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?

NOMINO

*Kielelezo Na.* 9: *Kichwa cha habari* kisicho sahihi.

Watahiniwa wengine walishindwa kutokana na kutokujua kusoma na kuandika, hivyo kushindwa kujibu swali kwa kuandika maneno yasiyoeleweka. Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika herufi zisizoeleweka badala ya kuandika kichwa cha habari kulinganana na matakwa ya swali.


41. Kichwa cha habari hii kingefaa kuwa kipi?

*Kielelezo Na.10*: *Majibu ya mtahiniwa asiyejua kusoma na kuandika.*


**Swali la 42:** Kwanini viongozi wengi wanawatumia wasanii kwenye mikutano yao?

Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa ufahamu. Jedwali Na. 34 linaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 42.

**Jedwali Na. 34: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa kwa kila Alama**

| Alama | 0.0 | 0.5 | 1.0 | 1.5 | 2.0 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 306,713 | 11,104 | 58,765 | 6,193 | 550,555 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 32.86 | 1.19 | 6.30 | 0.66 | 58.99 |


Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 615,513 sawa na asilimia 65.95 waliweza kutoa sababu sahihi za viongozi kutumia wasanii katika mikutano yao kuwa ni: *kuhamasisha watu kuhudhuria mkutano*. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya ufahamu na hivyo kusoma habari kwa umakini na kujibu maswali husika kwa usahihi. Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa ufasaha kulingana na kifungu cha habari alichosoma.


42. Kwanini viongozi wengi wanawatumia wasanii kwenye mikutano yao?

Kwa sababu wasanii huhamasisha watu waje kuwasikiliza kwenye miku-tano yao

*Kielelezo Na. 11: Sababu sahihi za wasanii kutumiwa katika mikutano.*

Aidha, watahiniwa 376,585 sawa na asilimia 34.05 walishindwa kutoa maelezo sahihi kwa kuwa hawakuwa na umakini katika kusoma habari na kutambua maudhui yaliyomo ndani yake. Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa stadi ya kusoma na kuandika hivyo kutokuelewa habari na kushindwa kuandika sababu za vingozi kuwatumia wasanii kwenye mikutano yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwa kutaja mito na maziwa mbalimbali tofauti na swali lilivyoulizwa. Kielelezo Na. 12 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali.


42. Kwanini viongozi wengi wanawatumia wasanii kwenye mikutano yao?

Kielelezo Na. 12: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa.*

**Swali la 43**. "Mwandishi anaposema "tuwaenzi wasanii" ana maana gani?"


Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kusoma habari kwa umakini. Jedwali Na. 35 linaonesha mtawanyiko wa alama za watahiniwa katika swali la 43.

**Jedwali Na. 35: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Alama**

| **Alama** | **0.0** | **0.5** | **1.0** | **1.5** | **2.0** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 393,655 | 7,725 | 15,7156 | 1,422 | 373,372 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 42.18 | 0.83 | 16.84 | 0.15 | 40.00 |

Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo watahiniwa 531,950 sawa na asilimia 56.99 walieleza kwa usahihi maana ya usemi "tuwaenzi wasanii" kuwa ni *kuwaheshimu/kuwapenda wasanii* kutokana na kusoma kwa umakini na kuelewa kifungu cha habari.


Hii inaonesha kuwa, Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kusoma kwa ufahamu hivyo waliweza kueleza maana mbalimbali za maneno yaliyotumika katika habari. Kielelezo Na. 13 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali.


43. Mwandishi anaposema "tuwaenzi wasanii" ana maana gani?

Tuwaheshimu wasanii

Kielelezo Na. 13: *Jibu sahihi la mtahiniwa.*

Aidha, watahiniwa 401,380 sawa na asilimia 43.01 walishindwa kueleza kwa usahihi maana ya usemi "tuwaenzi wasanii" jambo linaloonesha kuwa hawakuelewa kifungu cha habari walichopewa. Baadhi ya watahiniwa walitoa kauli mbalimbali zisizohusiana na swali na wengine walikosa stadi za kuandika na kusoma hivyo, kuandika maneno yasiyosomeka. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, "wanachama namna mbalimbali*,"* maneno ambayo hayakutumika katika habari aliyoisoma. Kielelezo Na. 14 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuandika maana ya "tuwaenzi wasanii" kama ilivyotumika katika habari.


43. Mwandishi anaposema "tuwaenzi wasanii" ana maana gani?

wanachama namna mbalimbali

Kielelezo Na. 14: *Jibu la mtahiniwa asiyefahamu maana ya usemi "tuwaenzi wasanii"*


**Swali la 44:** Katika aya ya tatu, mambo yapi mawili yamebainishwa kuwa yanachukiwa na wasanii?

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutumia maarifa na uelewa wa kifungu cha habari katika kubainisha mambo mawili yanayochukiwa na wasanii yaliyotajwa katika aya ya tatu katika kifungu cha habari. Jedwali Na. 36 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa.

**Jedwali Na. 36: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila chaguo**

| **Alama** | **0.0** | **0.5** | **1.0** | **1.5** | **2.0** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 102,775 | 212 | 46,664 | 1,456 | 782,223 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.01 | 0.02 | 5.00 | 0.16 | 83.81 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 830,343 sawa na asilimia 88.97 waliweza kubainisha kwa usahihi mambo mawili yanayochukiwa na wasanii katika aya ya tatu kuwa ni wizi na ufisadi. Hii inaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ufahamu hivyo kuweza kubaini wazo kuu katika aya ya tatu na kutoa majibu sahihi. Kielelezo Na.15 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


44. Katika aya ya tatu, mambo yapi mawili yamebainishwa kuwa yanachukiwa na wasanii?

(i) Wizi

(ii) Ufisadi

*Kielelezo Na. 15*: *Mambo mawili yanayochukiwa na wasanii.*

Aidha, watahiniwa 102,987 sawa na asilimia 11.03 walishindwa kubaini mambo mawili yanayochukiwa na wasanii kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma kifungu cha habari

kwa ufahamu. Baadhi ya watahiniwa walitaja aina za maneno na wengine walinakili baadhi ya maswali na kuyafanya kuwa sehemu ya majibu ya swali hili badala ya kubainisha mambo mawili yanayochukiwa na wasanii katika aya ya tatu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja baadhi ya mambo yaliyo katika aya ya pili badala ya aya ya tatu, hii inaonesha kuwa, mtahiniwa huyo hakuwa na uelewa wa msamiati wa neno *aya* hivyo kushindwa kutofautisha aya ya pili na aya ya tatu. Kielelezo Na.16 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini mambo mawili wanayochukia wasanii.

44. Katika aya ya tatu, mambo yapi mawili yamebainishwa kuwa yanachukiwa na wasanii?

(i) madini na

(ii) Waryama

*Kielelezo Na. 16: Majibu yasiyo sahihi kuhusu mambo yaliyobainishwa katika aya ya tatu.*


**Swali la 45:** Funzo gani unalipata kutokana na habari uliyosoma?

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kusoma habari, na kutumia maarifa na ueledi katika kubaini mawazo makuu ili kupata funzo. Jedwali Na. 37 linaonesha mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa.

**Jedwali Na. 37: Idadi na Asilimia ya Watahiniwa katika kila Alama**

| **Alama** | **0.0** | **0.5** | **1.0** | **1.5** | **2.0** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 285,959 | 6,400 | 108,910 | 2,131 | 529,930 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 30.64 | 0.69 | 11.67 | 0.23 | 56.78 |


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 640,971 sawa na asilimia 68.68 waliweza kubaini funzo linalopatikana katika kifungu cha habari kama vile: *Umuhimu wa wasanii katika jamii, madhara ya wizi na ufisadi na umuhimu wa wasanii katika kuitangaza nchi yetu*. Kielelezo Na. 17 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.


45. Funzo gani unalipata kutokana na habari uliyosoma?

Wasanii ni watu muhimu sana katika Jamii.

*Kielelezo Na. 17: kinaonesha funzo sahihi linalopatikana katika habari.*

Hata hivyo, watahiniwa 292,359 sawa na asilimia 31.32 walishindwa kueleza funzo linalopatikana katika kifungu cha habari kwa sababu walikosa maarifa ya kubaini maudhui katika kifungu cha habari walichosoma. Watahiniwa hao, waliandika majina ya wanyama na maneno yasiyokuwa na maana/yasiyo na upatanisho wa kisarufi na hivyo kutotoa ujumbe wowote kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika funzo ambalo halina uhusiano na habari aliyoisoma kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 18.


45. Funzo gani unalipata kutokana na habari uliyosoma?

walio Soma na Soma Mengi

malafiki wa kigombana ni fulaha kwa

*Kielelezo Na. 18: Majibu ambayo siyo funzo linalotokana na habari husika.*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mada zilizotahiniwa katika somo la Kiswahili ni *Sarufi*, *Lugha ya Kifasihi*, *Ushairi, Utungaji na Ufahamu*. Uchambuzi unaonesha kuwa, mada zote zilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Mada iliyokuwa na kiwango cha juu zaiidi ilikuwa ni *Lugha ya Kifasihi* (78.37%) ikifuatiwa na *Ufahamu (71.74%), Sarufi* (67.11%), Ushairi (64.03%) na Utungaji (61.35%). Uchambuzi wa kina unaonesha kuwa, maswali sita yaliyotahiniwa katika mada ya *Lugha ya kifasihi* yalijibiwa vizuri zaidi ambapo swali la 30 (92.13%), 21 (89.37%), 24 (89.31%), 22 na 25 (85.79%) na swali la 28 (84.24%) yalikuwa na wastani wa kufaulu zaidi ya asilimia 80. Katika mada ya *Ufahamu*, swali la 44 lilijibiwa vizuri zaidi na kuwa na wastani wa alama (88.97%). Aidha, katika mada ya *Sarufi*, swali la 5, 13, 6, 11 na 10 yalijibiwa vizuri sana ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa cha wastani wa zaidi ya asilimia 80 yaani (88.71%), (84.20%), (82.50%), (82.49%) na (81.10%) mtawalia. Pia katika mada ya *Ushairi* maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ni swali la 34 (84.52%) na 31 (82.14%) na katika mada ya *Utungaji* swali la 39 (82.18%) ndilo lililojibiwa vizuri zaidi.

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2018 na 2019 kinaonesha kupanda katika mada zote zilizotahiniwa kwa mwaka 2019*.* Viwango vya kufaulu kwa mwaka 2019 vikilinganishwa na mwaka 2018 vinaonesha kuwa; katika mada ya *Lugha ya Kifasihi* kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 70.89 hadi asilimia 78.37 sawa na ongezeko la asilimia 7.48. Pia, katika mada ya *Ufahamu*, kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 71.38 hadi 71.74 sawa na ongezeko la asilimia 0.36. Vile vile, katika mada ya *Sarufi* kumekuwepo na ongezeko la asilimia 10.04 kutoka (57.07%) hadi (67.11%). Pia katika mada ya *Ushairi*, kiwango cha kufaulu kimeongezeka kutoka

asilimia 58.81 hadi 64.03 sawa na ongezeko la asilimia 5.22. Kwa upande wa mada ya *Utungaji* kumekuwa na ongezeko la asilimia 4.21 kutoka (57.14%) hadi (61.35%).

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa mada unaonesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika mwaka 2019 ni kizuri zaidi ya mwaka 2018 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 5.46. Mwaka 2019 kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mada kilikuwa asilimia 68.52 ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo ni asilimia 63.06.

Uchambuzi huu umebainisha dosari zilizowafanya watahiniwa kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Miongoni mwa dosari hizo ni kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za msamiati, visawe na aina za maneno. Dosari nyingine ni kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika kujibu maswali mbalimbali.

Ili kukabiliana na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji, ni vema juhudi za makusudi zifanyike ili kuwawezesha watahiniwa kuwa na weledi wa kumudu somo la Kiswahili ambalo pia ni lugha ya Taifa na kielelezo muhimu cha utamaduni wa Mtanzania.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika somo la kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa dhana ya sarufi ili kuwajengea wanafunzi umahiri wa kubaini maana za msamiati, aina za maneno na kutumia aina mbalimbali za maneno kuunda sentensi kupitia mbinu za ufundishaji zifuatazo:
   (i) Mbinu shirikishi.
   (ii) Mbinu ya maigizo.
   (iii) Mbinu ya bungua bongo.

(b) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa mashairi kwa kuzingatia muundo wa utunzi wa shairi, maana ya msamiati na kughani mashairi kwa kutumia njia ya vikundi.

(c) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa matumizi ya lugha ya kifasihi katika methali, nahau, misemo na vitendawili hususani katika kuelewa maana, miundo na matumizi yake katika lugha ya Kiswahili.

**KIAMBATISHO A**

## ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2018 NA PSLE 2019

| Na | Mada | Mtihani wa 2018 | | | | Mtihani wa 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Kufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| 1. | Lugha ya Kifasihi | 21 | 83.90 | 70.89 | Vizuri | 21 | 89.37 | 78.37 | vizuri |
| | | 22 | 81.86 | | | 22 | 85.79 | | |
| | | 23 | 80.10 | | | 23 | 60.30 | | |
| | | 24 | 85.67 | | | 24 | 89.31 | | |
| | | 25 | 71.56 | | | 25 | 85.75 | | |
| | | 26 | 83.15 | | | 26 | 60.37 | | |
| | | 27 | 73.69 | | | 27 | 63.72 | | |
| | | 28 | 74.33 | | | 28 | 84.24 | | |
| | | 29 | 45.23 | | | 29 | 72.66 | | |
| | | 30 | 29.42 | | | 30 | 92.13 | | |
| 2. | Ufahamu | 41 | 86.78 | 71.38 | Vizuri | 41 | 78.28 | 71.74 | vizuri |
| | | 42 | 85.10 | | | 42 | 65.95 | | |
| | | 43 | 83.50 | | | 43 | 56.99 | | |
| | | 44 | 55.12 | | | 44 | 88.97 | | |
| | | 45 | 46.42 | | | 45 | 68.68 | | |
| 3. | Sarufi | 1 | 53.19 | 57.07 | Wastani | 1 | 44.15 | 67.11 | Vizuri |
| | | 2 | 30.24 | | | 2 | 52.65 | | |
| | | 3 | 54.27 | | | 3 | 30.30 | | |
| | | 4 | 88.44 | | | 4 | 75.61 | | |
| | | 5 | 51.05 | | | 5 | 88.71 | | |
| | | 6 | 74.94 | | | 6 | 82.50 | | |
| | | 7 | 45.34 | | | 7 | 35.59 | | |
| | | 8 | 52.94 | | | 8 | 45.45 | | |
| | | 9 | 55.28 | | | 9 | 59.02 | | |
| | | 10 | 52.46 | | | 10 | 81.10 | | |
| | | 11 | 66.30 | | | 11 | 82.49 | | |
| | | 12 | 45.71 | | | 12 | 73.27 | | |
| | | 13 | 62.74 | | | 13 | 84.20 | | |
| | | 14 | 46.09 | | | 14 | 78.90 | | |
| | | 15 | 31.00 | | | 15 | 77.01 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 16 | 72.37 | | | 16 | 79.09 | | |
| | | 17 | 48.32 | | | 17 | 72.78 | | |
| | | 18 | 60.79 | | | 18 | 78.79 | | |
| | | 19 | 71.05 | | | 19 | 49.75 | | |
| | | 20 | 79.01 | | | 20 | 70.75 | | |
| 4. | Ushairi | 31 | 74.33 | 58.81 | Wastani | 31 | 82.14 | 64.03 | vizuri |
| | | 32 | 36.97 | | | 32 | 77.49 | | |
| | | 33 | 76.96 | | | 33 | 60.40 | | |
| | | 34 | 74.12 | | | 34 | 84.52 | | |
| | | 35 | 20.51 | | | 35 | 47.81 | | |
| | | 36 | 69.99 | | | 36 | 31.91 | | |
| 5. | Utungaji | 37 | 46.77 | 57.14 | Wastani | 37 | 47.19 | 61.35 | vizuri |
| | | 38 | 61.78 | | | 38 | 53.06 | | |
| | | 39 | 45.38 | | | 39 | 82.18 | | |
| | | 40 | 74.63 | | | 40 | 63.03 | | |

**KIAMBATISHO B**

**MUHTASARI WA ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA PSLE 2018 NA 2019 KWA SOMO LA KISWAHILI**

